# UTANGULIZI

Tume ya Pamoja ya Fedha ni Taasisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 134 na kuanzishwa kupitia Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Sura 140. Jukumu la msingi la Tume ni kutoa ushauri na mapendekezo kuhusu Uhusiano wa Kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Aidha, Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 kupitia Ibara ya 124 inatambua mamlaka ya Tume ya Pamoja ya Fedha kutekeleza majukumu yake Zanzibar. Tume ilianza kutekeleza majukumu yake mwaka 2003.

## MREJESHO NI NINI?

Mrejesho ni taarifa anayotoa Mwananchi kuhusu huduma anayopatiwa na Taasisi ya Umma. Mrejesho unaweza kuwa Malalamiko, Mapendekezo, Maulizo, au Pongezi.

## MWANANCHI NI NANI?

Mwananchi ni mtu yeyote anayepata huduma katika Taasisi ya Umma.

### MISINGI YA KUSHUGHULIKIA MREJESHO

Mrejesho utashughulikiwa kwa kuzingatia misingi ya: Uwazi, Usiri, usawa na Kujali muda kwa kushughulikiwa kwa wakati. Lengo kuu ni kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa Wananchi na kuongeza uwazi katika utoaji wa huduma.

## NJIA ZITAKAZOTUMIKA KATIKA KUTOA NA KUPOKEA MREJESHO

(i) Maandishi
(ii) Simu
(iii) Ana kwa Ana
(iv) Sanduku la Maoni
(v) Dawati au Ofisi ya mrejesho
(vi) Ubao wa Matangazo
(vii) Mifumo ya TEHAMA na tovuti
(viii) Barua pepe
(viii) Sanduku la Posta

## UTOAJI WA MAJIBU YA MREJESHO

Tume itaandaa na kutoa majibu ya Mrejesho uliopokelewa ndani ya muda uliokubalika katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja.
Mkataba wa huduma kwa Mteja wa Tume katika Kipengele cha 6.5 umeeleza viwango vya utoaji huduma kama ifuatavyo:-

i. Tutafanya mawasiliano na kujibu hoja mbalimbali za wateja hususani katika uhusiano wa kifedha kwa pande mbili za Muungano ndani ya siku tano baada ya kupokea hoja.
ii. Tutajibu maswali ya waandishi wa habari kwa maandishi ndani ya siku saba za kazi baada ya kuyapokea.
iii. Tutakiri kupokea barua zinazohitaji ufafanuzi ndani ya siku tatu za kazi baada ya kupokelewa.
iv. Tutajibu barua zinazohitaji ufafanuzi ndani ya siku saba za kazi.
v. Tutatoa huduma ya mawasiliano ya kiofisi kwa wateja kwa utaratibu wa barua pepe ndani ya siku tano za kazi.

## FAIDA ZA MREJESHO

### FAIDA KWA MWANANCHI

i. Kuwa na fursa ya kutuma, kupokea na kufuatilia Mrejesho kuhusu huduma zinazotolewa na Serikali.
ii. Kupunguza muda wa Utafutaji na ufuatiliaji wa huduma za Serikali.
iii. Kuongeza uelewa kuhusu huduma zinazotolewa na Serikali.
iv. Kumwezesha Mwananchi kushiriki katika kuboresha utoaji wa huduma za Serikali.

### FAIDA KWA SERIKALI

i. Kurahisisha utoaji wa huduma kwa Umma.
ii. Kuimarisha nidhamu, uadilifu na uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma.
iii. Kuongea uwazi na uwajibikaji wa Taasisi kwa Wanachi.
iv. Kuboresha Mipango ya Serikali kufikia malengo ya kitaifa.
v. Kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza gharama za utoaji huduma za Serikali.
vi. Kuimarisha Utawala Bora.
vii. Kuendeleza mahusiano mazuri baina ya Serikali na Wananchi.

## FAIDA KWA TAASISI

i) Kurahisisha utoaji wa huduma kwa Umma

ii) Kuboresha utendaji kazi wa Watumishi wa Umma

iii) Kuimarisha nidhamu, uadilifu, kwa Watumishi wa Umma

iv) Kupata fursa ya kutuma, kupokea na kufuatilia mrejesho kuhusu huduma zinazotolewa na Serikali; na

v) Kupunguziwa gharama na muda wa utafutaji na ufuatiliaji wa huduma za kiutumishi.

## UPATIKANAJI NA UJAZAJI WA FOMU YA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA MREJESHO

**Upatikanaji**

i) Mratibu wa Mrejesho/ Ofisi ya Mrejesho

ii) Dawati la Mapokezi

iii) Sanduku la maoni limewekewa sehemu ya kuhifadhi fomu za Mrejesho.

iv) Tovuti ya Tume (kwa kupakua fomu)

## UJAZAJI

Fomu ya Mrejesho ijazwe na kuwekwa/kukabidhiwa kwa Mratibu wa Mrejesho/Ofisi ya Mrejesho, Dawati la Mapokezi, Sanduku la Maoni au kujaza katika eMrejesho kupitia Tovuti ya Tume.

## USHUGHULIKIAJI WA MREJESHO

Dawati/Ofisi ya Mrejesho itakusanya fomu hizo kwa wakati na kuzifanyia uchambuzi na kuwasilisha kwa Mratibu wa Mrejesho ili kutoa ushauri kwa Menejimenti.

Tume ya Pamoja ya Fedha inawakaribisha Wananchi na Wadau wote kutoa Mrejesho kuhusu huduma zinazotolewa na Tume. Pia tunawakaribisha kusoma Mkataba wa Huduma kwa Mteja unaopatikana katika tovuti yetu.

## WASILIANA NASI


Barua pepe: **katibu@jfc.go.tz**

Tovuti: **www.jfc.go.tz**

Simu: **+255-22 2120576**


## OFISI ZETU ZINAPATIKANA


Jengo la Sukari (Sukari House)-Mtaa wa Sokoine/Ohio

S. L. P. 9281

DAR ES SALAAM

Jengo la ZSTC-Mtaa wa Gulioni

S. L. P. 1796

ZANZIBAR


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA PAMOJA YA FEDHA

# FAHAMU UTARATIBU KUHUSU UTOAJI WA MREJESHO WA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA TUME

JANUARI, 2024